

ASANTE MUNGU WANGU

Gosbert Damazo

A sa nte Mungu wangu A sa nteMunguwangu (A)A sa nteMunguwangu

4 MASHAIRI

A sa nte

1. a)Uliniumbakwakwa ulinipe nda kwa ni ni Munguwangu ni si kushuku ru
b)Ulinipa vi umbe vyote vyadunia kwa ni ni Munguwangu ni sikushuku ru

1. a)Uliniumba kwa kuwa ulinipenda, kwa nini Mungu wangu nisikushukuru
b)Ulinipa viumbe vyote vya dunia, kwa nini Mungu wangu nisikushukuru.

2. a)Wanipa ulinzi usiku na mchana, kwa nini Mungu wangu nisikushukuru
b)Unanipa kinga nao waovu wote, kwa nini Mungu wangu nisikushukuru.

3. a)Unanifahamu nisivyojifahamu, kwa nini Mungu wangu nisikushukuru
b)Ninayoyawaza unayajua yote, kwa nini Mungu wangu nisikushukuru.

4. a)Bwana ni chakula na tena ni kinywaji, kwa nini Mungu wangu nisikushukuru
b)Unawashibisha wanaokuhitaji, kwa nini Mungu wangu nisikushukuru.